# UBATIZO HALISI WA ROHO MTAKATIFU

*Yohana Mt. 3:3-8 Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuingia ufalme wa Mungu*

Kwamba, Roho Mtakatifu anapaswa kuwa wa muhimu sana kwako kuliko kitu kingine chochote kile duniani; heshima yako, maisha yako, kazi yako, chochote kile cha kwako ulicho nacho. Usitulie mpaka umempata huyo. Lazima umpokee. Lazima iwe ya ………….. Na unasema vema nawaogopa wale pale kazini kwangu. Naogopa mume wangu, jamani …………… usiogope; Liache hilo liwe la kwanza. Achilia kitu kingine chochote kiende. Liache hilo liwe la kwanza". Vema, nategemea kumpata huyo katika moja ya siku hizi. Ndugu Branham. Siyo siku moja ya siku hizi; sasa, huu ndio wakati na liwe hilo ni la kwanza kabla sijafanya kitu kingine chochote. Na niwe naye sasa". Kutaharuki. Hiyo itasaidia kujibu swali letu. Unapokuwa …………… unapotaharuki juu yake. Umpate au ufe, hapo ndipo utaenda kumpata.

Kama nilivyosema usiku uliopita kuhusu kisima cha chemchemi ya maji kumwagilia mazao yako au kama umesimama hapa katikati ya shamba, na kumekuwa na giza zito, na useme oh umeme ulio mkuu, najua uko hapa shambani sasa. Sasa nimepotea, sijui ninakokwenda. Nipe nuru, ili niweze kuona namna nitakavyotembea. Kuna umeme utoshao kuangazia shamba; hiyo ni kweli ndiyo Bwana kuna umeme wa kutosha kuangaza hiki chumba bila hata hizi taa. Bila hizo. Lakini yapasa uziongoze. Sasa, unaweza kupiga kelele sana mpaka usiweze tena kupiga kelele, tena; katu hautatoa nuru. Lakini kama utafanya sawasawa na kanuni za umeme, hapo sasa utapata nuru.

Vema, hivyo ndivyo ilivyo na Mungu. Mungu ni muumbaji mkuu wa mbingu na dunia, Yule jana leo na hata milele. Yeye bado ni Mungu. Lakini Yeye atatenda kazi tu kwa kadiri unavyofuata sheria Zake na maagizo. Marafiki, nasema hivi: sijaliona likishindwa na naamini haliwezi kushindwa.

Sasa, hebu tuangalie Yesu katika Luka 24:49 alikuwa amewapa agizo wale mitume baada ya kuwa wameokolewa na kutakaswa kulingana na Neno. Kuhesabiwa haki kwa kumuamini Bwana Yesu Kristo; kutakaswa kwa Yohana 17:7 Yesu aliposema watakase Baba, kwa ile kweli, kweli ni Neno lako" Naye alikuwa ni Neno.

Sasa, aliwapa nguvu kuponya wagonjwa, kutoa pepo, kufufua wafu nao wakarudi wakifurahia (Matayo 10:1; Luka 10:17-20). Na majina yao yalikuwa yameandikwa kwenye kitabu cha uzima cha mwana kondoo. Mnakumbuka tumekwisha kulipitia hilo sasa. Lakini wao walikuwa bado hawajaokolewa. Yesu akamwambia Petro usiku ule wa kusulubishwa. Akasema baadaye ukiokolewa/ukibadilishwa, waimarishe ndugu zako" (Luka 22:31-32).

Unaamini kwa ajili ya uzima wa milele. Lakini Roho Mtakatifu anapokuja, huo ni uzima wa milele (Yohana 5:24). Wewe uko tu kifuani kwa baba unapotakaswa, lakini hata hujazaliwa kwa Roho mpaka Roho Mtakatifu aje ndani. Hiyo ni sahihi. Mtoto ana uhai akiwa tumboni mwa mama, misuli midogo ile ikicheza; ni uhai. Lakini ni uhai wa tofauti anapovuta hewa ya uhai kupitia pua zake. Hiyo ni tofauti. Hivyo ndivyo ilivyo ni …………..

Mpendwa ndugu yangu wa Methodist, na Pilgrim Holiness na wanazarene, ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tofauti na utakaso. Utakaso ni kusafishwa, ambayo ni maandalizi ya uhai. Lakini Roho Mtakatifu anapokuja ni uhai. Maandalizi ni kukisafisha chombo; Roho Mtakatifu ni kukijaza chombo. Kutakaswa maana yake ni kusafishwa na kuwekwa kando kwa huduma. Roho Mtakatifu ni kukiweka kwenye huduma (1Kor. 12:4-6). Wewe ni chombo Mungu alichokisafisha.

Sasa, angalia kuhesabiwa haki hakukumwingiza Yeye ndani. Kutakaswa kulisafisha tu sehemu ya Yeye kukalia. Lakini ulipokuja Ubatizo wa Roho Mtakatifu, ulimweka Yeye ndani ya watu.

Hebu tutafute kile Biblia inasema sasa. Tunaona katika 1Kor.12:13 Biblia ilisema "Kwa Roho mmoja sisi wote tulibatizwa katika mwili mmoja". Tumebatizwa ndani ya mwili wa Kristo kwa Roho Mtakatifu mmoja. Sio kwa kutingishwa, sio kwa kujiunga, sio tumeingizwa kwa kubatizwa kwa maji. Tumebatizwa kwa Roho Mtakatifu ndani ya mwili wa Yesu Kristo.

"Sasa, basi hakuna hukumu (hapana hukumu ya kidunia, hawawezi wakakuhukumia cho chote) ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu ambao hawaendi kwa kuufuata mwili, bali kufuata Roho (Rumi 8:1).

Hiyo ndiyo namna ya kuhukumu ukristo wako. Hiyo ndiyo namna ya kujua kwamba umeingia katika lile pumziko; Dunia haikusumbui tena. Hakika, unaiona, unatembea mbali nayo. Una kitu bora cha kufikiria juu yake. Tuko pale. "Hakuna hukumu ……." Hivyo ndivyo tunavyoingia ndani ya mwili. Na unakuwa salama milele (Waef. 4:30) Biblia ilisema hivyo.

Moja ya kweli za kimungu zilizofunuliwa katika wakati huu: Siri ya ubatizo wa Roho Mtakatifu bila misisimko, lakini utu wa Kristo ukitenda kazi ndani yako kazi zile zile alizozitenda. Nini? Kanisa, hiyo ndiyo maana siwezi kuchukua ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa kulia, kutetemeka au kunena kwa lugha au

moja ya misisimko. Hayo yote ni mazuri sasa unaona? Hayo mambo ni mazuri, lakini shetani anaweza kuyaigiza hayo yaonekane halisi.

Lakini Roho Mtakatifu ni Uungu, Mungu akikaa ndani ya watu. Hiyo ni zaidi ya msisimko. Ni zaidi ya kuzungumza kwa lugha. Ni zaidi ya kupiga kelele katika Roho. Ni zaidi ya kulia. Ni zaidi ya kujiunga na kanisa. Ni Mungu akiishi ndani ya watu, Uungu, Mungu mwenyewe akikaa ndani ya mtu, Anapozungumza inakuwa tu ni sawa na Mungu aliyezungumza; hilo ndilo kanisa la Yesu Kristo.

Sasa, siyo lazima ubatizwe (na maji) ili kupokea Roho Mtakatifu kwa sababu unaweza kupokea Roho Mtakatifu moyo wako ukiwa uko sahihi. Unaona? Kwa sababu katika Matendo 2:37 – 41 Petro alitoa njia ya "Kutubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu". Lakini tena, katika Matendo 10:44-48. Mungu aligeuka na kuwapa watu wa mataifa ubatizo wa Roho Mtakatifu kabla hata hawajabatizwa. Unaona? Kwa hiyo unaona ni ile hali ya moyo wako.

Ndipo Petro akasema, ni nani awezaye kuzuia maji, kuona kwamba watu hawa wamepokea Roho Mtakatifu kama tulivyopokea pale mwanzoni? Unaona? Hivyo aliwahimiza kwamba ni lazima wabatizwe katika Jina la Yesu Kristo.

Yeye anaikomboa dunia sawasawa na vile anavyomkomboa mtu. Mtu anaamini nini? Anaamini, halafu anabatizwa, halafu anaoshwa kwa damu, anatakaswa ambao ni ujumbe wa Wesley. Halafu anajazwa na moto wa Roho Mtakatifu na kuondoa dunia ndani yake; na amejazwa na moto wa Roho Mtakatifu, ambaye ni Neno (au ubatizo wa Roho Mtakatifu na Neno: Yohana 6:63). Unaamini hilo? Sasa angalia vile Mungu anavyoenda kukomboa dunia yake kwa njia ile ile.

Mungu anatenda kazi katika utatu: kuhesabiwa haki kwa imani, kutakaswa, na kukaa Yeye mwenyewe ndani ya watu wake kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Jambo lile lile. Shetani yuko akiwa ni mwigizaji mfano baada ya Kristo oh. Shetani naye hukaa ndani ya watu.

Wakati Yesu Kristo anapokaa Mwenyewe ndani ya watu wake. Maisha yale yale yaliyokuwa ndani ya Kristo yanakuwa ndani ya huyo mtu. Maisha yanaelezea ni kitu gani. Unaona?

Wakati unaposikia watu wanasema wanaye Roho Mtakatifu na wanakataa hili Neno, kuna kitu sio sahihi. Roho Mtakatifu aliandika Neno (2Petro 1:20-21). Na Yesu alisema hivi: "Kama mtu ana Roho Wangu ndani yake atafanya kazi zangu" (Yohana 14:12).

Sasa, angalia sasa Yesu aliwaambia (Luka 24:49) na tazama nawaletea juu Yenu ahadi ya Baba yangu lakini mwende Yerusalemu na mngoje hata ……….."

Ahadi ya Baba ilikuwa ni nini? Joeli 2:28-32, kwa nini? Tunaona alikuwa anaenda kuwamwagia Roho Mtakatifu. Katika Isaya 28:11, jinsi ambavyo kwa midomo ya kugugumiza na lugha ngeni na mambo haya yote. Walienda juu pale na kama tulivyolipitia hilo ……….
Pengine mmoja angalisema "kwa nini, Naamini tumengoja muda mrefu wakutosha. Natulipokee hilo kwa imani". Hayo ni mafundisho mazuri ya kibaptisti. Lakini haikuweza kutenda kazi na hao ndugu. Kwa hiyo, kitu cha kwanza unajua, inabidi iwe ni kitu halisi, na wao walingoja katika huduma yao hata lile Neno lithibitishwe. Na unapomtafuta Roho Mtakatifu fanya jambo hilo hilo.

Ndiyo, unaweza kulipokea kwa imani, inabidi umkubali Kristo kwa imani; hiyo ni sawa kabisa. Na unampokea Roho Mtakatifu kwa imani, Lakini sasa acha Roho Mtakatifu aje na kukupa Kutahiriwa kama shahidi kwamba ameikubali imani yako (Waefeso 1:13 –14) unaona?

Ona, Ibrahim alimuamini Mungu na ikahesabiwa kwake kuwa ni haki, lakini Mungu alimpa yeye ishara ya kutahiriwa kama uthibitisho kwamba ameikubali imani yake (Warumi 4:9-12). Kwa hiyo tunapaswa kufanya jambo hilo hilo. Tumsubiri Roho Mtakatifu mpaka awe amefanya jambo fulani, siyo lazima kwa sababu tumenena kwa lugha, siyo kwa sababu tumecheza au tumepata msisimko, tumepiga kelele: Ni mpaka tuwe tumebadilika, mpaka jambo fulani hasa limetukia. Sijalishi linakuja kwa namna gani, ili mradi tu liwe limetokea; hilo ndilo la Muhimu.

Na ninaamini juu ya kunena kwa lugha na mambo haya yote ni sawa. Lakini hilo tu halitaweza kusimama, na unajua halitasimama. Kwa hilo halifanyi hivyo. Nimeona wachawi wakinena kwa lugha, nimeona walozi wakinena kwa lugha, na kucheza katika Roho. Unaona? Hakika wanailaza penseli chini na inaandika kwa lugha ngeni na mwingine anatafsiri hilo (unaona hiyo ni kweli) na kusema kweli. Hiyo ni sawa inaandika kwa usahihi jambo lilitokea na ni sawa kabisa iko hivyo.

"Nijaponena kwa lugha za wanadamu na za malaika kama sina upendo, hainisaidii kitu" (1Kor. 13: 1 – 3) unaona? Ingawa naweza kufanya hilo. Unaona? Kwa hivyo mambo hayo hayamaanishi kuwa unaye Roho Mtakatifu. Lakini Yeye, ule utu, yule Roho wa milele wa Kristo anapokuwa mwokozi wako binafsi, na kukubadilisha wewe, na kuelekeza mawazo yako moja kwa moja msalabani, kwenye hili Neno, jambo fulani limetokea. Ndiyo Bwana. Jambo fulani limetokea. Hakuna anayepaswa kukuambia juu ya hilo; utajua hilo pale linapotokea.

Na Divai mpya, inapoleta ufunuo, hapo limefunuliwa, na hivyo ndivyo ilivyokuwa wakati wa Pentekoste. Walijua kuwa Roho Mtakatifu angemwagwa juu yao nao walingojea mpaka jambo hilo likatokea. Na wakati uthibitisho wa ufunuo ulipofanyika, ndipo uamsho ukaja juu yao.

Kwa hakika walifanya. Walichemka pia. Moja kwa moja mitaani, walipokuwa wanaogopa na milango imefungwa, na sasa wako mitaani. Walikuwa wanaogopa vikundi vya watu, wakihubiri injili kwao. Hiyo ni kweli unaona? Kuna jambo limetokea, kwa sababu Neno la kweli la ahadi lilithibitishwa (Matendo 2:1-36).

Swali: wakati ule wa kupokea Roho Mtakatifu, au ubatizo wa Roho Mtakatifu, je kuna tofauti? Je mtu ananena kwa lugha? Kama sio siku zote, kuna udhihirisho gani unaojulikana?

Vema, unaweza kuwazia mama anayejifungua mtoto naye asijue hilo? Inabidi awe hana fahamu ili asijue hilo.

Kadhalika haiwezekani upokee Roho Mtakatifu bila kujua hilo. Kuna kitu fulani kinatendeka ndani yako, unaona? Kuna kitu fulani kinakubadilisha. Utu wako wote, utu wako wote wa kiroho unafanywa upya tena, na unakuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo, kama Biblia inavyoliweka hilo, kiumbe kipya ndani ya Kristo (2Kor.5:14) unajua hilo.

Sasa unasema Ndugu Branham, kwa hiyo huamini kuwa mtu lazima azungumze kwa lugha ili kupokea Roho Mtakatifu? Siyo kithibitisho kuwa ana Roho Mtakatifu.

Ningependa kila mshiriki wa kanisa langu anene kwa lugha, ningependa wao wafanye hivyo, na ninaamini ukimuomba Mungu, Mungu atakupatia hilo. Lakini ngoja nikuambie wewe; ninawajua watu wengi wanaonena kwa lugha na hawana Roho Mtakatifu. Na hakuna mhudumu ambaye ni mkweli kwa nafsi yake na kusanyiko lake ila atakaye.

waambia watu wake jambo hilo hilo. Shetani anaweza akaigiza hilo. Paulo alisema hilo katika 1Kor 13: 1-10 ……… Lakini ijapo ile iliyo kamili iliyo kwa sehemu itabatilika au wakati ile iliyokamili itakapojulikana.

Kanisa limeanguka kupitia kuhesabiwa haki kwa imani, Martin Luther; kupitia utakaso, Wesley, lakini ilipofikia wakati wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, walionyesha rangi zao; hawahitaji chochote kuhusiana na hilo. Wanazarene Pilgrim holiness, Kanisa la Mungu, wote wale walioamini juu ya utakaso, hawawezi kunyosha kidole kwa hilo. Ni kweli, lakini inapokuja ni mstari wa mpakani, wanakuja mpaka pale mahali pa kupokea Roho Mtakatifu kwa ajili ya kuzaliwa mara ya pili hapo shetani atafanya nini? Atakuja na kulipindisha pindisha. Oh atafanya kila awezalo ambalo liko katika uwezo wake unaojulikana kuwazuia watu wasifike nje pake.

Wakati wote uliopita walipokea Roho Mtakatifu, lakini siyo katika kiwango/kipimo tulichonacho sasa; kwa sababu ni wakati wa kurudishiwa kile cha mwanzoni (Malaki 4:5-6). Sasa, lakini katika wakati huu wa kanisa ule ujumbe unamiminiwa na kumwagwa Kanisani. Lakini kanisa lenyewe kwa namna ya mwili, juu yote ……….. kama maskani hii, watasema hapo ndipo atakapokuja kanisani. Maskani hii siyo maskani ya Roho Mtakatifu. Hakuna kitu kama hicho. Watu binafsi wanaokuja hapa kanisani ndio Roho Mtakatifu. Hao ndio maskani ambazo zinaye Roho Mtakatifu ndani yao. Lakini siyo kanisa kama jengo ila kundi la watu.

Nabii alisema mwishoni mwa ujumbe! Nampenda Yeye ……… imba hilo kwa vyote ulivyo navyo moyoni, sikia kile kitu halisi kitamu/kizuri kizuri kinachokujia; huyo ni Roho Mtakatifu.

Halafu anaomba: Nijaze mimi na Roho. Nipe ishara ya upendo wako juu yangu, Roho Mtakatifu, ambaye atanifanya niishi kwa utamu, upole. Nifanye niishi maisha yaliyo kuwa ndani ya Kristo, kwamba moyo wangu utawaka kwa ajili ya wengine, kwamba sitaweza kutulia usiku na mchana, mpaka nimempata kila mmoja niwezaye kumpata.

Roho Mtakatifu ni ishara kwamba Damu imepakwa ndani ya moyo, na ni ishara kwamba damu imepakwa. Kama haijapakwa, hapo ile ishara haiwezi kuja (Kutoka 12:13) mnaelewa semeni Amina. Damu lazima ipakwe, na hapo ile ishara inakuja ni ishara ya kuwa ile Damu ya ukombozi imepakwa na gharama imelipwa. Mungu awabariki.

Nukuu za Kiingereza:
Maswali na majibu (59-1223) COD uk. 483/maswali na majibu juu ya Roho Mtakatifu COD Uk. 416/mahali Bwana alipochagua pa kuabudia (65-0425) aya 95/waebr.sura ya 4 uk. 154 aya 209/je hii ni ishara ya wakati wa mwisho. Bwana uk. 31/ushuhuda wa shahidi wa kweli uk. 186/Nawezaje kushinda uk. 49
Maswali na majibu (54-0103m) COD uk. 65/wakati wa mavuno aya 333/mhuri wa pili
K.Mihuri uk 204-205/mhuri wa nne uk. 289 – 290/maswali na majibu (64-0823E)
COD uk. 1016 Swali no. 289/maswali na majibu (64-0830m) COD uk. 1124 majina ya makufuru uk. 19/ile ishara (63-0901M) uk.61.

---

Jiwe la kiroho la kujengea no. 130 kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa hii yamekusanywa na Gerd Rodewald Friendestr.69 D 75328 Schomberge Germany
Phone (+49) 72357613 Fax 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyo chaguliwa kimbele imesikia. [Nd. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724]

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*